TANGAZO LA SERIKALI NA. 925 la tarehe 22/12/2023

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya Kifungu cha 7(1) na 16(1))*

MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA USHURU WA ZAO LA MKONGE YA HALMASHAURI YA WILAYA YA KOROGWE YA MWAKA 2023

Jina

TS Na. 196 la 2020

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Ushuru wa Zao la Mkonge ya Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe ya Mwaka 2023, na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya Ushuru wa Zao la Mkonge ya Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe ya mwaka 2020, ambayo hapa imerejewa kama "Sheria Ndogo Kuu".

Marekebisho ya aya ya 4

2. Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa kwa kufuta aya ya 4 na kuiandika kama ifuatavyo:

> "4. Halmashauri itatoza ushuru wa zao la mkonge kwa kiwango cha asilimia tatu (3%) ya bei ya shambani kutoka kwa kila mnunuzi wa zao hilo kwenye eneo la Halmashauri ."

Marekebisho ya aya ya 6

3. Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa katika aya ya 6(a) kwa kufuta neno "mauzo" na badala yake kuweka neno "shamba".

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya Korogwe imegongwa kwenye sheria Ndogo hii kufutia azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe uliofanyika Tarehe 5/11/2021 na Kushudiwa na Lakiri hiyo ikigongwa mbele ya :-

GOODLUCK A. MWANGOMANGO
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe*

KALLAGHE S. YUSUPH
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe*

NAKUBALI,

Dodoma,
31 Oktoba, 2023

MOHAMED OMARI MCHENGERWA (MB)
*Waziri wa Nchi – Ofisi ya Rais,*
*(Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa)*